



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO



Tarehe: 11/05/2024

**TAARIFA KWA UMMA  
KUHUSU ULIPAJI WA KODI YA PANGO LA ARDHI**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro inapenda kuajulisha Wananchi wote, Makampuni, Taasisi za Serikali na Binafsi kuwa, kwa mujibu wa Kifungu cha 33 (1) cha Sheria ya Ardhi (Sura ya 113), kila mmiliki wa ardhi amepewa sharti la kulipa kodi ya Pango la Ardhi kwa kila mwaka.

Aidha, kwa **Kifungu cha 44 (1) cha Sheria ya Ardhi (Sura ya 113)**, kila mmiliki wa ardhi anatakiwa kutimiza masharti ya umiliki ikiwa ni pamoja na sharti la kulipa Kodi ya Pango la Ardhi. Kitendo cha kutolipa Kodi ya Pango la Ardhi ndani ya muda uliowekwa na sheria, kinasababisha mmiliki wa ardhi kuvunja moja ya sharti la umiliki.

Halmashauri kwa nyakati tofauti, imekuwa ikihamasisha na kuwakumbusha wamiliki wa ardhi kulipa Kodi ya Pango la Ardhi. Hata hivyo, baadhi ya wamiliki wa ardhi hawajatekeleza wajibu huo wa kisheria. Hivyo, inaelekezwa wamiliki wote wa ardhi wanaodaiwa Kodi ya Pango la Ardhi, kulipa kodi husika ndani ya siku thelathini (30) kuanzia tarehe ya tanagazo hili. Baada ya muda huo kupita, hatua za kisheria zitachukuliwa katika maeneo yafuatayo:

- Kwa mujibu wa **Kifungu cha 50 cha Sheria ya Ardhi (Sura ya 113)**, wamiliki hao watafikishwa mbele ya Mahakama; na
- Kwa mujibu wa **Kifungu cha 45 cha Sheria ya Ardhi (Sura ya 113)**, taratibu za kisheria za ubatilisho wa milki zao zitaendelea.

Katika kipindi hicho cha siku thelathini (30), Ofisi za Ardhi za Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, zitakuwa wazi kwa siku za kazi kuanzia Asubuhi hadi muda saa 3:00 Usiku. Hivyo, Wananchi na wamiliki wote wa ardhi mnakaribishwa kukamilisha malipo haya ya kodi ya Pango la Ardhi kwa muda mabao umetolewa.

”Lipa Pango la kodi ya Ardhi kuchangia Pato la Taifa”

**IMETOLEWA NA:  
KITENGO CHA MAWASILIANO YA SERIKALI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO**